VIGEZO NA MASHARTI YA KUZINGATIA WAKATI WA KUSHIRIKI MBIO ZA KILIMANJARO PREMIUM LAGER MARATHON, TIGO KILI HALF MARATHON AU MBIO KUU ZA MALT FUN.

Ninathibitisha kuwa nimesoma na kuelewa kikamilifu na kukubali "vigezo na masharti" kama yalivyo katika fomu hii, na ninathibitisha kwamba nina vigezo vya kushiriki na kushindana kama ilivyofafanuliwa na sheria ya shirikisho la Riadha Tanzania. Kwa kusaini fomu hii ninakiri sitakuwa na madai ya fidia dhidhi ya Kilimanjaro Marathon, wafanyakazi wao au mawakala wao kutokana na hasara au majeraha yatakayotokana na na mimi kushiriki mbio hizo. Ninathibitisha kuwa ninakidhi vigezo vya kusaini fomu hii ya usajili na kukubaliana na vigezo na masharti yafuatayo:-

1. Ninatambua na kukubaliana kwamba tukio la michezo lililoandaliwa na/au kusimamiwa na mratibu wa tukio ("tukio") ni tukio ambalo linajumuisha adhari za kiasili, kuumia, ugonjwa, kifo na /au uharibifu wa mali kwa washiriki, michezo na vifaa vingine.

2. Ninakiri kuwa na ufahamu kuhusu hatari au athari zinazoweza kujitokeza wakati wa kushiriki tamasha la mbio hizi, ambazo zinaweza kuwa nje ya uwezo au ujuzi wangu au kwa mshiriki mwingine, zinazoweza kusababishwa na lishe yangu na unywaji wa maji, mazoezi yangu ya viungo na afya kabla na wakati wa tukio, eneo ambalo tukio hilo linapita, hali ya barabara, hali ya hewa, hali ya maji, vyombo vya moto, vitendo vya washindani wengine, mratibu wa tukio, wadhamini na wakuu wao, wawakilishi, mawakala na wenye dhamana ya tukio. Ninakiri kwamba nitajitoa kushiriki tukio ikiwa nitashauriwa au kuagizwa na mratibu wa tukio kufanya hivyo au nitakvyoona inafaa, wakati wowote nitakapobaini hali yoyote isiyo ya kawaida au isiyo salama na nikawa na wasiwasi kwamba si salama kwangu kushiriki tukio hili.

3. Ninatambua kwamba tukio hili linaweza kufutwa kutokana na majanga ya asili yaliyo nje ya uwezo wa mratibu wa tukio (ikiwa ni pamoja na: athari za kimazingira, mgomo, vita, ghasia, moto, mafuriko, mabadiliko ya kisheria, uasi, mlipuko wa magonjwa, vikwazo vya serikali na/au migogoro ya kibiashara) na kwamba katika mazingira kama hayo, mratibu wa tukio hatawajibika kurejesha ada ya kiingilio. Ninakiri kuelewa athari hizi na ninashiriki kwa ridhaa yangu mwenyewe na endapo nitadhurika sitakuwa na madai yoyote dhidi ya waandaji, wawakilishi, wadhamini, washiriki wengine au mawakala wao.

4. Ninakiri kwamba nitafuata sheria, kanuni na maelekezo yote nitakayopewa na mratibu wa tukio wakuu wake, wawakilishi na mawakala na kwamba tukio limeratibiwa kwa mujibu wa kanuni za shirikisho la riadha la kimataifa (IAAF) na shirikisho la kimataifa la riadha na mbio ndefu (AIMS) na shirikisho la riadha la Tanzania.

5. Ninaelewa kwamba ninaweza kupigwa picha na/au kuchukuliwa filamu kabla, wakati au baada ya tukio. Ninakiri Kwamba waandaji wa tukio, wadhamini, wakuu wao, wawakilishi wao, na mawakala wao wanaweza kutumia picha au filamu hizo katika jambo lenye mahusiano na tukio hilo au tukio lijalo.

6. Ninakiri kwamba, kutokana na ushiriki wangu katika tukio hilo, waandaaji wa tukio hilo wanaweza kuwasiliana nami mara kwa mara (kwa njia ya barua pepe, ujumbe mfupi na/au simu) kwa madhumuni ya:

    i. Kuwasilisha taarifa zinazohusiana na tukio;
    ii. Kutangaza bidhaa fulani na / au huduma ambazo zinaweza kunisaidia katika maandalizi yangu katika kushiriki tukio; na / au
    iii. Matangazo ya riadha na / au matukio mengine ya mbio yaliyoandaliwa na / au kusimamiwa na mratibu wa tukio. Ninakiri nitakubali mawasiliano yoyote kama hayo.

7. Wazazi au walezi wanaoidhinisha ushiriki wa watoto katika tukio hili, watatakiwa kudhibitisha ushiriki wao kwa kutia saini zao katika fomu za ushiriki, na kwamba kwa kufanya hivyo watakuwa wamekubaliana na kufungwa na masharti haya. Vivyo hivyo washiriki watakaoruhusu watu wenye umri mkubwa (wazee) kushiriki tukio hili watafungwa na masharti haya.

8. Kwa kusaini fomu ya ushiriki ninathibisha kwamba sitakuwa na madai yoyote ya kisheria dhidi ya waandaji wa tukio yatokanayo na majanga ya asili, hasara yoyote, majeraha, madhara, Ugonjwa, kifo au uharibifu uliotokea moja kwa moja au nje ya tukio ikiwa ni pamoja na uzembe wa washiriki, au madai yoyote ya upotevu wa mali, madai yatokanayo na kupoteza faida au madai yoyote ya wategemezi wangu yanayotokana na matukio yanayohusiana na, ushiriki wangu katika tukio hili.

9. Ninathibitisha kwamba ninaelewa umuhimu na maana ya kanusho hili la dhima, kutokuwa na madai, na kwamba kwa kukubaliana hapa, ninathibitisha sitakuwa na madai ya kisheria (kwa niaba yangu mwenyewe na kwa niaba ya wategemezi wangu). Ninakiri kwamba nina uhuru wa kupata ushauri wa kisheria binafsi kabla ya kushiriki tukio kwa mujibu wa masharti yote ya kanusho hili la dhima, na kwamba ichukuliwe nimechukua ushauri wa kisheria na / au ushauri mwingine kabla ya kushiriki tukio.

10. Ninakiri kuwa na uelewa kwamba kwa kushiriki Tamasha la mbio za Kilimanjaro Marathoni, ama fun run hakutakuwa na mrejesho wa fedha za kiingilio, kuchagua mtu mbadala wa kushiriki, au kuwakilishwa na mtu mwingine kutokana na kiingilio kilichokwisha lipwa.

11. Washiriki wanakiri, na kuridhia kwamba Tamasha linaweza kuahirishwa endapo kutatokea jambo ambalo litazuia kuendelea kwa tamasha kutokana na vitu vilivyo nje ya uwezo wa binadamu kama majanga, mgomo, vita, ghasia, moto, mafuriko, machafuko ya wenyewe kwa wenyewe, mabadiliko ya kisheria, uasi, mlipuko wa magonjwa, vikwazo vya kiserikali na mzozo wa kibiashara. Hivyo kwa mazingira hayo, waandaji wa Tamasha hawatawajibika kurejesha fedha za kiingilio.

12. Washiriki wanakubali kwamba, wakati wa kushiriki mbio watatumia vifaa vya kujikinga binafsi (PPE) vitakavyotolewa kwa maelekezo yatakayotolewa na waandaaji wa Mbio hizi sambamba na kuchukua tahadhari dhidi ya maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa Corona (Covid-19) kwa kiwango kinachokubalika kimataifa, ikiwa ni pamoja na kutotangamana na watu katika maeneo yaliyoanishwa kwa ajili ya kuanza mbio siku ya tukio.